OFISI YA RAISI – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SEKONDARI KURASINI
S.L.P 50008, DAR ES SALAAM. TANZANIA
SIMU : +255713 365 385, +255712 170 800.

JINA LA MWANAFUNZI ……

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHKE YA SEKONDARI KURASINI ILIYOPO MANISPAA YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA – 2021

UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha …… katika Shule ya Sekondari Kurasini ambayo ipo km 3 kutoka katikati ya jiji la Dar es salaam kupitia barabara ya Kilwa kituo cha Mabasi kiitwacho Mivinjeni. Shule itafunguliwa tarehe ……..

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. **SARE ZA SHULE**

A) Kwa Wavulana, sare ya Shule hii ni suruali 2 rangi ya kijivu **zisizobana (Modo**). Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa suruali inayobana **yaani (MODO**). Upande wa chini wa suruali usiwe chini ya nchi 16 (isibane miguu hadi usawa wa chini wa goti hadi paja – isibane mwili urefu wa suruali ifikie kwenye kifundo cha mguu au suruali iguse kiatu.
Kwa wasichana sketi 2 za rangi ya kijivu urefu ufikie chini ya magoti au kwa watakao shona sketi ndefu, urefu ufikie kwenye kifundo cha mguu. Mshono wa sketi unaitwa linda boksi.

B) Mashati 2 meupe mikono mifupi na mkanda mweusi wa ngozi kwa wavulana na kwa upande wa wasichana, mashati 2 meupe ya mikono mifupi au nusu kanzu nyeupe isiyobana yenye mikono mirefu. Hijabu nyeupe inayoziba sehemu ya tumbo na sio kifua tu**. (si ruhusa kusuka au kuwa na nywele ndufu)**

C) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba (gidamu) na vyenye visigino vifupi kwa wavulana na wasichana.

D) Soksi ndefu (free size) za rangi nyeupe (zisichanganyike na rangi yeyote) kwa wavulana na wasichana.

NB : Sare ya Shule itavaliwa kila siku za masomo na siku za mapumiziko (jumamosi, Jumapili, Sikukuu) pindi mwanafunzi anapotakiwa kuwepo eneo la Shule au kwenye mikutano au maazimisho ya Sherehe za Kiserikali au Kidini zinazofanyika siku za mapumziko.

2. **VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI**

A. Madaftari makubwa 12 Counter book quire 3 na peni
B. Mkebe wa hesabu (Mathematical set) na rula ndefu ya cm 30
C. Begi la shule la kubeba mgongoni

D. Brashi ya viatu na kiwi nyeusi, Mkebe mdogo
E. Kitambaa cha mkononi (Leso / Hengachifu)

3. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya RAIS – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo.

a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kil ashughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili mavazi na mazingira ya Shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakwa
h) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma

4. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Kukutwa na vitu vyenye ncha kali mfano (Kisu, wembe, bisibisi n.k)
e) Kuruka ukuta au kupita sehemu isiyostahiki
f) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
g) Kupigana au kupiga
h) Kubaribu kwa makusudi mali ya umma
i) Kudharau bendera ya Taifa
j) Kuwa mjamzito / kupata mimba
k) Kutoa mimba
l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu.
m) Kukataa adhabu kwa makusudi
n) Kuwa na simu ya mkononi
o) Kutoa lugha ya matusi kwa mtu yeyote
p) Utoro sugu
q) Kucheza mchezo wa kamali
r) Kuchora au kuandika kwenye kuta / mali za Shule

5. MIPAKA YA SHULE

Shule ya Sekondari Kurasini imezungushiwa uzio wa ukuta. Upande wa Mashariki imepakana na Shule ya Msingi Mivinjeni. Upande wa Magharibi imepakana na nyumba za makazi ya wafanyakazi wa Shirika la Reli (TRC) upande wa kaskazini imepakana na Barabara inayounganisha Barabara ya KIlwa na Barabara ya Shimo la udongo na upande wa Kusini imepakana na nyumba za makazi ya wafanyakazi wa Shirika la Reli (TRC)

6. RUHUSA YA KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE

a) Ruhusa ya kutoka nje ya shule kwa muda tu au siku inatolewa na Mwalimu wa darasa. Mwalimu wa zamu kwa pasi (kibali maalumu)
b) Ruhusa ya kutoka nje ya Dar es salaam itatolewa na Mkuu wa Shule au Makamu kwa pasi (kibali maalumu). Apatapo ruhusa ya nje ya Shuel, mwanafunzi anapaswa kuwahi kurudi
c) Ruhusa ya kwenda hospitali inapatikana kwa kupewa kibali na Mwalimu wa darasa au Mwalimu wa zamu.

7. MAHUDHURIO

a) Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vya masomo vya ndani na nje ya darasa kama ilivyoonesha kwenye ratiba.
b) Wanafunzi wote wanatakiwa kuhuduria na kushiriki katika shughuli zote za shule kama vile baraza la shule ukaguzi wa usafi. Kupandisha Bendera ya Taifa na kazi za mikono
c) Ni lazima kutii kengele au wito wa shughuli yoyote ya shule kwa haraka na bila kuchelewa
d) Kuhudhuria zamu za shule za mwisho wa wiki au likizo
e) Utoro wa rejareja na wa kudumu (utoro sugu) utapelekea mwanafunzi kufukuzwa shule.

8. MALI NA VIFAA VYA SHULE

Wanafunzi wote wanatakiwa kutunza kwa uwezo wote mali na vyombo vya shule vilivyo chini ya uangalizi wao.

a) Hakuna chombo au kifaa cha aina yoyote kinachoruhusiwa kutoka mahali pake kwa matumizi au shughuri zisizo idhinishwa
b) Iwapo chombo kimeamishwa kwa shughuli maalumu ni lazima kirudishwe mahali pake mara tu baada ya matumizi husika.
   Uharibifu au upotevu wa kifaa chochote cha Shule makusudi ama uzembe lazima ulipiwe na muhusika.

9. MATIBABU

a) Huduma ya kwanza itatolewa shuleni
b) Inapobidi kwenda nje ya shule kwa ajili ya matibabu ni lazima kuwa na ruhusa kutoka kwa Mwalimu wa zamu.
c) Shule haitawajibika na gharama zilizotumika / zitakazotumika kumtibu mwanafunzi katika Zahanati / Hospitali ya binafsi / Serikali nje ya Shule.

10. LUGHA YA MAWASILIANO

Lugha rasmi kwa maandishi au kwa kuzungumza shuleni na Kiingereza. Hivyo tumia kiingereza wakati wote.

11. VITU VISIVYORUHUSIWA

1. Pete
2. Kunyoa nyusi
3. Herein
4. Kupaka rangi
5. Rangi ya kucha
6. Kucha ndefu
7. Kupaka piko (rangi nyeusi) kwenye nywele / upara
8. Kukali au kulitachi ni marufuku
9. Hairuhusiwi kunyoa mtindo
10. Hairuhusiwi kunyoa vipara
11. Hairuhusiwi kuwa na nywele ndefu au kusuka nywele
12. Hairuhusiwi kuvaa mabuti na viatu vinavyofanana na jeshi
13. Hairuhusiwi kuvaa sandozi, mikanda na vazi rasmi la shule
14. Mashati makubwa sana na slim fiti hayaruhusiwi
15. Simu ya mkononi
16. Kuja na redio shuleni
17. Kuja na game shuleni
18. Kuvaa suruali zinazobana **(modo)**
19. Kuvaa sketi zinazobana na fupi (juu ya goti) sketi ziwe chini ya goti

12. SHERIA YA JUMLA

Kila wakati fikiria kwanza kabla ya kunena na tumia busara kutenda.

13. MAMBO MENGINEYO MUHIMU YANAPAWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

a) Fomu ya kundikishwa shuleni (Maelezo ya mwanafunzi na Mzazi / Mlezi). Kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
b) Fomu ya kukubali kujiunga na shule na ahadi (yaani kufuata sharia kanuni na taratibu za shule)
c) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

TAFADHALI SOMA KWA MAKIN MAELEZO / MAAGIZO HAYA NA KUTATEKEZA KIKAMILIFU

KARIBU SANA KURASINI SEKONDARI

……
AMRY J FUNDI
MKUU WA SHULE

KIAMBATANISHO A

OFISI YA RAISI – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SEKONDARI KURASINI

FOMU YA KUANDIKISWA SHULENI
IJAZWE NA MWANAFUNZI

1. JINA LA KAMILI LA MWANAFUNZI ……
2. TAREHE YA KUZALIWA …….
3. URAIA ……..
4. DINI ……..
5. SHULE ALIYO SOMA KABLA YA KUJA SHULE YA SEKONDARI KURASINI.

SHULE YA MSINGI	TAREHE NA MWAKA ULIANZA	TAREHE NA MWAKA ULIOTOKA

SAINI YA MWANAFUNZI ……. TAREHE ……

B: **MAELEZO BINAFSI YA MZAZI / MLEZI**

1. JINA KAMILI LA MZAZI / MLEZI ……
2. URAIA ……
3. ANUANI YA MZAZI / MLEZI ……
4. SEHEMU ANAYOISHI ……..
5. MTAA ……
6. NAMBA YA NYUMBA ……...
7. SIMU MKONONI
   I) BABA ……
   II) MAMA ……
   III) NDUGU MWENGINE ……..

ELEZA KAMA MTOTO ANA MATATIZO YOYOTE YA KIAFYA

……
……

C : **MAELEZO YA KIKAZI**

I) JAZA JINA LA MWAJIRI ……
II) KAZI YA MZAZI / MLEZI ……..

SAINI YA MZAZI / MLEZI …… TAREHE ……

KIAMBATANISHO B

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KURASINI
S.L.P 50008
DAR ES SALAAM.

A: KWA MWANAFUNZI

Mimi …….. …….. jina kamili Ninakubali nafasi niliyopewa na kuingia kidato cha …….. mwaka …….. katika shule ya sekondari Kurasini

NINAAHIDI KWAMBA

1. Nitatii sharia za shule kama nilivyozisoma
2. Nitaweka bidii katika masomo, kazi na shughuli zote za kishule
3. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali, kuzalisha mali ilivyo bora bila kuitia hasara shule kwa kuharibu au kupoteza mali ghafi (raw materials) ya uzalisha mali
4. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu mkakamavu mwenye mwenendo safi wakati wowote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kulipa na kutunza sifa ya shule ya Sekondari Kurasini.

MUNGU NISAIDIE

SAINI YA MWANAFUNZI …… TAREHE ……

B : **KWA MZAZI / MLEZI**

Mimi ……. Jina kamili

NAAHIDI KWAMBA

1. Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yalivyotajwa katika maelezo ya kujiunga na Shule
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaotajwa (maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu
3. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (home work) na kufuatilia maendeleo yake shuleni. Ikiwa ni pamoja na kukagua madaftari yake mara kwa mara
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake
5. Nitahakikisha mwanangu anavaa sare kama iliyoelekezwa na hasa kwa wasichana sketi isiwe fupi (kimini) yaani isiwe juu ya goti na kwa wavulana suluari isiyobana (modo)

SAINI YA MWANAFUNZI …… TAREHE ……

KIAMBATANISHO C

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

STATION …….

DATE ……

PART A
TO
MEDICAL OFFICER
……

…….

MISS / MR. ……...

Please examine above named as to his / her fitness for admission as a student in the following common diseases / problems

Put a tick (v) for positive and cross (x) for negative in a box provided

Pregnancy	
Asthma	
Diabetes	
Worms (stool)	
Epilepsy	
TB (tuberculosis)	
Sickle cell	
Heart Disease	
Yellow fever	
U.T.I	
Malaria	

PART B

MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by a Medical Officer)

I Have examined the above namedand consider that she / he is physically FIT / UNFIT for admission above.

Date …….. Signature ……
Station …….. Designation ……